MFUMO WA STAKABADHI ZA GHALA KATIKA SEKTA NDOGO YA KAHAWA

UTANGULIZI

Maana ya mfumo:-

a. Ni utaratibu unawezesha biashara kufanyika kwa kutumia bidhaa ambazo zinakua zimehifadhiwa kwenye ya ghala lilopewa leseni kwa mujibu kifungu cha 5 (a) cha Sheria Namba 10/2005 na marekebisho yake Namba 3/2015;

b. Mmiliki wa Bidhaa / Mazao bidhaa anapewa stakabadhi ambayo inathibitisha Ubora, Uzito, Idadi ya Vifungashio, na za umiliki mahususi.

c. Stakabadhi inayotolewa inaweza kutumika kwa ajili kuhifadhi, biashara na kupata mkopo kutoka katika asasi za fedha.

MFUMO WA STAKABADHI ZA GHALA

Utekelezaji wa Mfumo Katika zao la Kahawa

1. Mwaka 1999 Kwa **majaribio** katika Maeneo Mbali mbali – Kilimanjaro, Mbeya, Mbinga, na Kigoma;
2. Mwaka 2007 Kisheria Baada ya kupata **Sheria Namba 10 ya 2005** na Kanuni za **Stakabadhi za Ghala 2006** – Kilimanjaro, Mbeya, Mbinga, Mara na Kagera;
3. Katika zao la Kahawa matumizi ya Mfumo kwa sasa ni kwa **hiari** kwa wale wanaotaka kama **vikundi vya wakulima**, **Vyama vya Ushirika vya Msingi na** kampuni za watu binafsi
4. Kwa sasa mfumo umetekelezwa kwa **miaka 11** ukiwa na takwimu kama Jedwali namba 1 linavyoonyesha

MFUMO WA STAKABADHI ZA GHALA

Jedwali Na 1 : Utekelezaji wa Mfumo katika Zao la Kahawa

Na	Mwaka	Kahawa		Jumla Kuu		Mchango
		Gunia	Kilo	Gunia	Kilo	(%)
1	2007/2008	29,769	1,488,430	793,822	62,580,053	2.40%
2	2008/2009	12,643	632,156	711,144	56,594,630	1.10%
3	2009/2010	143,546	7,177,291	1,164,056	86,521,831	8.30%
4	2010/2011	144,592	7,236,423	1,897,724	141,511,941	5.10%
5	2011/2012	69,709	4,186,796	2,128,842	168,267,153	2.50%
6	2012/2013	178,265	10,695,899	1,672,788	130,177,912	8.20%
7	2013/2014	90,962	5,457,722	1,504,421	118,495,482	4.60%
8	2014/2015	113,634	6,818,011	2,282,256	180,460,522	3.80%
9	2015/2016	147,879	7,393,938	1,806,991	140,232,229	5.30%
10	2016/2017	141,971	7,098,513	3,265,802	257,282,293	2.80%
11	2017/2018	-	-	3,640,306	291,614,066	0.00%
	Jumla Kuu	**1,072,970**	**58,185,179**	**17,227,846**	**1,342,124,046**	**4.30%**

Chanzo: WRRB, 2018

MFUMO WA STAKABADHI ZA GHALA

MAMBO YA KUZINGATIA KWA SASA

1. Kuzingatia Sheria ya Stakabadhi Namba **10 ya Mwaka 2005** na marekebisho yake **Namba 3/2015;**
2. Kanuni za Stakabadhi za ghala za **Mwaka 2016;**
3. Mwongozo **Namba 5 wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala Toleo la 2** wa Zao la Kahawa ambao unatambua na kukubali mambo makuu yafuatayo:-
   i. Kuweka bayana **Wadau Wakuu** katika Mfumo;
   ii. **Kuondoa migongano baina ya taasisi** katika utekelezaji wa Mfumo;
   iii. **Kutambua uwepo wa sheria nyingine** kama Sheria ya Vipimo Viwango, Chakula na Lishe, Serikali za Mitaa n.k;
   iv. **Kubainisha viwango** vya utendaji kwa kila Mdau Mkuu.
4. Matumizi ya **nyaraka zote za ndani** zilizobainishwa kwenye Sheria, Kanuni na Mwongozo.

MFUMO WA STAKABADHI ZA GHALA

…/MAMBO YA KUZINGATIA KWA SASA

Wadau Wakuu

1) *Mweka Bidhaa* ni Chama cha Ushirika Cha Msingi

a)Ndiye Mmiliki halali Bidhaa (Kahawa) kwa niaba ya wanachama na wasio wanachama;

b)Stakabadhi itaandikwa kwa kila chama husika;

c)Malipo yote ya Bidhaa (Kahawa) yatafanyika kupitia akaunti ya benki ya chama husika;

d)Kama kuna haja Mkopo kwa ajili ya Biashara hii ndicho kitakachokopeshwa;

e)Faida au hasara ya chama kimoja haitanufaisha au kuadhiri chama kingine

2) *Mwendesha Ghala* ni Viwanda vyote vya kukobolea Kahawa

a)Bodi ya usimamizi wa Stakabadhi za Ghala watatoa Leseni kwa Ghala la Kuhifadhia Kahawa ya Maganda au Buni;

b)Stakabadhi itaandikwa kwa idadi na uzito wa kahawa ya Maganda au Buni;

c)Vigezo vyote vya kuhakiki ubora na uzito ni jukumu la Mwendesha Ghala

d)Mwendesha ghala atawajibika kwa tofauti ya Ubora na Uzito kama ulivyobainishwa kwenye stakabadhi na vile viwango vya kitaifa vilivyopo

3) *Wanunuzi wa Kahawa Safi*

a)Wanunuzi wote wa kahawa safi wa nje na wa ndani

b)Wanunuzi wote watanunua kahawa kutoka Mnadani kwa taratibu za mnada

c)Watachukua kahawa safi kwa Mwendesha ghala kutoka kwa Mwendesha Ghala baada ya kukamilisha taratibu zote za malipo.

MFUMO WA STAKABADHI ZA GHALA

…/MAMBO YA KUZINGATIA KWA SASA

Mamlaka za Usimamizi za Serikali

1. *Bodi za Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala;*

   i. watatoa leseni kwa ghala zote za kuhifadhi kahawa za maganda (Ngumu na Laini);

   ii.Ndio wasimamizi wakuu wa kahawa ya maganda katika ghala walizotoa leseni;

2. *Bodi ya Kahawa Tanzania*

   i. watatoa leseni kwa viwanda vyote vya kukobolea kahawa

   ii. watatoa leseni kwa ghala zote za kuhifadhi kahawa safi;

   iii. Ndio wasimamizi wakuu wa kahawa safi katika ghala walizotoa leseni;

   iv. Watatakiwa kuendelea kutambua stakabadhi ya ghala iliyotolewa katika ghala la kuhifadhi kahawa za maganda.

MFUMO WA STAKABADHI ZA GHALA

…/MAMBO YA KUZINGATIA KWA SASA

Mamlaka za Usimamizi za Serikali

3. Tume ya Ushirika Tanzania na Maafisa ushirika katika Wilaya

i. Kuratibu huduma zote za wakulima kukusanya kahawa;

ii. Kuratibu mchakato wote wa mikopo ya kibenki ambayo itahitajika kwa ajili ya kuwezesha makusanyo kufanyika;

iii. Kuratibu malipo yote kwa wakulima wote watakaopeleka kahawa katika vyama vya ushirika vya msingi

4. Serikali za Mitaa, Mikoa na Serikali Kuu

i. Ndiyo wasimamizi wakuu sera na sheria zote

ii. Kuhakikisha kuwa wakulima na wadau wengine wote wamelipwa katika maeneo yao ya utawala

MFUMO WA STAKABADHI ZA GHALA

Mamlaka za Usimamizi za Serikali

5. Taasisi nyingine zinazotoa huduma

i. Wakala wa Vipimo Tanzania;

ii. Mamlaka ya Mapato Tanzania;

iii. Mamlaka ya Bandari

Taasisi binafsi zitakazotumika

i.Benki za Biashara

ii.Kampuni za Bima

iii.Wasafirishaji

iv.Wagavi

v.Kampuni za Habari na Mawasiliano

MFUMO WA STAKABADHI ZA GHALA

Mambo yanayoweza kukwamisha utekelezaji wa Mfumo:-

i. Matukio yoyote ya kughushi katika ghala zilizopewa leseni;

ii. Asasi za fedha kutokutoa mikopo ya malipo ya awali;

iii. Kahawa kuuzwa na malipo kutokufanyika kwa chama husika

iv. Vyama vya Ushirika kuamua kutumia fedha za wakulima bila kuwashirikisha wakulima wote. **NB Stahiki ya chama cha Ushirika cha Msingi ni ushuru wake tu. Fedha nyingine zote ni mali ya mkulima;**

WRRB
WAREHOUSE RECEIPTS REGULATORY BOARD